



TAARIFA KWA UMMA

Kumekuwa na taarifa inayosambaa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu kufungwa kwa benki ya **Amana (Amana Bank Ltd)**.

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuufahamisha umma kuwa taarifa hiyo ni ya uzushi. Benki ya Amana inaendelea kufanya shughuli zake kama kawaida na hivyo wateja wa benki hiyo na umma kwa ujumla waendeleo kutumia huduma za benki hiyo kama kawaida.

Benki Kuu inatoa rai kwa watumiaji wa mitandao ya kijamii kuacha mara moja kusambaza taarifa za uzushi kwa kuwa taarifa kama hizo zina madhara makubwa na ni kinyume cha Sheria. Benki Kuu kwa kushirikiana na vyombo vya usalama haitasita kuchukua hatua za kisheria dhidi ya mtu yeyote au chombo chochote cha mawasiliano kitakachosambaza taarifa za uzushi.

BENKI KUU YA TANZANIA

17 Novemba 2017